# Watoto wanaozungumza lugha nyingi na lugha mbili: manufaa na changamoto

**Inafaa kwa**
**0-18**
**miaka**

**https://raisingchildren.net.au/newborns/connecting-communicating/bilingualism-multilingualism/bilingualism**

## Mambo makuu

- **Iwapo unajua lugha mbili, unazungumza kwa kutumia lugha mbili. Iwapo unajua lugha nyingi, unazungumza kwa kutumia zaidi ya lugha mbili.**
- **Kulea watoto wanaojua lugha nyingi au lugha mbili kuna manufaa mengi. Kwa mfano, kunaweza kuunda mahusiano thabiti wa kifamilia na ya kitamaduni.**
- **Kulea watoto wanaojua lugha nyingi au lugha mbili kuna changamoto nyingi. Kwa mfano, kunaweza kuchukua muda mwingi na wakati mwingi.**

## Manufaa ya kuwalea watoto wanaojua lugha nyingi au lugha mbili

Kulea watoto wanaojua lugha mbili au lugha nyingi ni vizuri sio kwa watoto wako pekee, bali pia kwa familia na jamii yako.

**Watoto: manufaa ya kujua lugha nyingi au lugha mbili**
Kwa watoto, kuzungumza lugha zaidi ya moja kunahusishwa na:

- matokeo mazuri ya kimasomo – hii ni kwa sababu watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili wanaweza kumakinika vizuri zaidi, wanaweza kutatua matatizo vizuri zaidi, wanaelewa miundo ya lugha vizuri, na wanajua kutekeleza shughuli mbalimbali wakati mmoja
- Wanapata nafasi nyingi na tofauti za kiajira baadaye katika maisha.

Pia, iwapo watoto wako walikua wakizungumza lugha zaidi ya moja, wanaweza **kujiona watu wa maana, kujihisi wako na utambulisho na hisia za kukubalika**. Hili linatokana na:

- Kuhisi vizuri kuhusu urithi wao
- kuhisi wanajiamini katika kuwasiliana na kuingiliana na wanafamilia wa ukoo na watu wanaozungumza lugha nyinginezo


© Raising Children Network

- wanaweza kufurahia muziki, sinema, fasihi na kadhalika kwa lugha zaidi ya moja.

**Familia: manufaa ya kujua lugha nyingi na lugha mbili**
Kwa familia yako, kujua lugha nyingi na uendelezaji wa lugha yako kwa watoto wako:

- kunaimarisha mawasiliano miongoni mwa wanafamilia wako
- kunaimarisha mahusiano ya kihisia
- kunakurahisishia wewe pamoja na watoto wako kuwa sehemu ya utamaduni
- kunakuza hisia za familia yako za utambulisho na ufaafu.

**Jamii: manufaa ya kujua lugha nyingi na lugha mbili**
Kwa jamii yako pana, watoto wanapozungumza lugha zaidi ya moja, inamaanisha kuwa:

- kila mtu katika jamii anakubali vizuri zaidi uzungumzaji wa lugha tofauti na tamaduni mbalimbali
- watoto wanaweza kusafiri kwa urahisi na kufanya kazi katika mataifa tofauti na tamaduni wanapokua
- watoto wanaelewa na kukubali vizuri zaidi tamaduni tofauti

## Changamoto zinazoweza kutokea za kuwalea watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili

Kulea watoto wanaojua lugha nyingi au lugha mbili kuna changamoto zake, ikiwa ni pamoja jinsi ya kukabiliana na **shinikizo za kuzungumza Kiingereza pekee**. Pia kunaweza kumaanisha kazi nyingi, na wajibu wa muda mrefu.

Kwa mfano, unapowalea watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili, unahitajika:

- kudumisha lugha yako ya utamaduni, hata kukiwa na shinikizo la kuchagua lugha ya Kiingereza
- kujiweka pamoja na watoto wako mkiwa na motisha wa kutumia lugha za kitamaduni
- kuwasaidia watoto wako kuelewa manufaa ya kujua lugha nyingi na lugha mbili
- kuhakikisha kuwa watoto wako wanapata nafasi nyingi za kusikia na kutumia lugha yao ya pili na pia lugha nyinginezo
- kuzungumza na walimu wa watoto wako na kupata usaidizi wao katika jitihada zako


© Raising Children Network

- kujitafutia usaidizi – kwa mfano, kwa kuzungumza na marafiki na familia ambao wanalea watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili na kutafuta raslimali katika jamii yako, kama vile chekechea za masomo ya lugha mbili.

Iwapo mara nyingine unahisi kuwa changamoto hizi ni ngumu sana, inaweza kusaidia kufikiria kuhusu manufaa ya kujua lugha nyingi – hasa jinsi ambavyo kunaweza kukusaidia pamoja na watoto wako kudumisha mahusiano ya kifamilia. Kusaidiana, kushauriana na uzoefu na wazazi wengine pia kunaweza kuwa na usaidizi mkubwa.

## Kujua lugha nyingi au lugha mbili: maswali yanaoyoulizwa sana

**Je, watoto wanaweza kuelewa tofauti zilizoko katika lugha?**
Watoto wanaweza kuelewa tofauti kati ya lugha katika umri mchanga na kujifunza lugha mbili au zaidi kwa wakati mmoja. Kwa mfano, wanatambua kwa haraka zaidi kuwa wanafaa kuzungumza Kijerumani wanapozungumza na nyanya yao, na kuzungumza Kiingereza wanapozungumza na mwalimu wao.

**Je, kujua lugha nyingi au lugha mbili kutaathiri jinsi ambavyo watoto wanasoma Kiingereza?**
Watoto wanaolelewa katika familia ambapo wazazi wana ufahamu mdogo wa lugha ya Kiingereza wanafanya vizuri katika usomaji wa lugha ya Kiingereza wakiwa shuleni iwapo wanazungumza lugha za familia wakiwa nyumbani. Hii ni kwa sababu msingi thabiti wa lugha yao ya mama unafanya iwe rahisi kujifunza lugha ya pili.

**Je, kujua lugha nyingi au lugha mbili kutaathiri vipi ujuzi wa msingi wa kusoma na kuandika?**
Watoto wanaojua lugha nyingi au lugha mbili ambao wanatumia lugha zaidi ya moja iliyoandikwa – kwa mfano, Kihispania na Kiingereza – au hata mifumo tofauti ya uandishi – kwa mfano, Kichina na Kiingereza – wanaweza kusoma na kuandika Kiingereza katika hali ya juu. Pia wanaweza kuwa na uelewa bora zaidi wa uhusiano kati ya jinsi maneno yanavyokaa na yanavyotamkwa zaidi ya marafiki zao wanaozungumza Kiingereza peke yake.

**Je, kujua lugha nyingi au lugha mbili kunaathiri vipi uendelezaji wa usemi?**
Watoto wote wanaimarika katika usemi katika viwango tofauti. Usomaji wa lugha zaidi ya moja katika wakati mmoja hakutaathiri iwapo mtoto wako atajua kuzungumza mapema au kwa haraka. Wakati mwingine watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili wanachanganya lugha zao kwa wakati, ila hili linajitatua baada ya wao kutambua kuwa wanazungumza kupitia lugha zaidi ya moja.


© Raising Children Network